

Wataalam wa Marekani kutoa huduma bure ya meno Ruvuma

Na Furaha Thonya

WATAALAMU wa tiba ya Meno kutoka katika Shirika lisilo la kiserikali la Marekani Miracle Corners of the World (MCW) wanatarajia kutoa huduma za meno bure kwa wakazi wa Mkoa wa Ruvuma.

Taarifa iliyotolewa na Ubalazi wa Marekani inasema kuwa mbali na kutoa huduma hiyo wataalamu hao wanatarajia kufanya shughuli za kujitolea kwa wakazi wa Mikoa ya Iringa na sehamu mbalimbali za Jiji la Dar es Salaam.

Mbali na kutoa huduma ya meno, MCW itawaelimisha wakazi wa mikoa mbalimbali katika masuala ya Elimu, Afya, Uchumi na miradi ya maendeleo endelevu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa (MCW), Edward Bergman, ujumbe huo umeambatana na Madakari watatu kutoka katika Chuo Kikuu cha New York, wanafunzi watano kutoka katika chuo hicho na madaktari wawili kutoka Afrika Kusini.

Aliongeza kusema kuwa katika Mkoa wa Ruvuma Madaktari hao watawatibu wakazi wenye matatizo mbalimbali ya meno kwa kushirikiana na madaktari wa hospitali ya Mkoa.

Aidha Bw. Bergman ameongeza kuwa madaktari hao watatumia vifaa walivyokuja navyo kutoka Marekani na vile walivyoviacha katika ziara kwenye hospitali hiyo mwaka uliopita.

Bw. Bergman alisema kuwa

wanatarajia kuendeleza kiasi cha hekta 50 ambazo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa ofisi katika mkoa wa Ruvuma kwenye Shirika, ambazo zina makao makuu ya Ofisi katika mkoa wa Arusha.

Pia alisema kuwa kituo hicho kitakuwa na mradi wa ufugaji na vile vile, kitajenga nyumba zenye gharama nafuu kwa ajili ya vijana katika mkoa huo.

Wakitokea Songea wataalam hao watakwenda Iringa kufanya tathmini ya ujenzi wa maktaba ya Chuo Kikuu cha Kanisa Katoliki cha Iringa, Bw. Bergman alisema.

Pia ujumbe huo utatembelea Ofisi kuu zilizoko mjini Arusha na wataangalia upya ufanisi wa Kituo kilichopo Majengo ambacho kilijengwa kwa msaada wa MCW.

Kituo hicho kinachojulikana kwa jina la Dk. Herman Wrice Youth Village Community Centre kinasaidia wakazi wapatao 1,000 kwa mwaka, Bw. Bergman alieleza.

Hata hivyo, ujumbe huo pia ulitembelea Shule ya Msingi Abdulwakil iliyopo Mpiji-Magohe jijini Dar es Salaam.

Mbali na Tanzania, MCW imeendeleza miradi mbalimbali katika nchi za Ivory Coast na Siera Leone.

Kadhalika, MCW imeandaa mipango ya Kimataifa kwa ajili ya uongozi kwa vijana, ambayo itatoa mafunzo na uwezeshaji wa mawasiliano ya kiutamaduni katika Nchi zilizoko Afrika na katika Bara la Amerika.